JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA YA TANZANIA

# HOTUBA YA MHE. PROF. IBRAHIMU HAMIS JUMA, JAJI MKUU WA TANZANIA SIKU YA SHERIA NCHINI TAREHE 01 FEBRUARI 2023

## HOTUBA YA MHE. PROF. IBRAHIMU HAMIS JUMA, JAJI MKUU WA TANZANIA SIKU YA SHERIA NCHINI TAREHE 01 FEBRUARI 2023

Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Wahe. Majaji wa Mahakama ya Rufani,

Mhe. Khamis Ramadhan Abdallah, Jaji Mkuu wa Zanzibar,

Mhe. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi,

Mhe.Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria,

Wahe. Majaji wa Mahakama Kuu,

Wahe. Majaji Wakuu wastaafu na Majaji Wastaafu

Mhe. Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali,

Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania,

Mhe. Wilbert Chuma, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania,

Wakuu wa vyombo vya Ulinzi na Usalama,

Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika,

Wahe. Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa,

Wasajili, Wakurugenzi na Watendaji wa Mahakama,

Mahakimu na Mawakili,

Viongozi wa vyama vya Siasa,

Viongozi wa Dini.

Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana.

# 1. UTANGULIZI:

Kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana hapa leo tukiwa na afya njema. Kwa niaba ya Mahakama ya Tanzania nakushukuru wewe Mhe. Rais kwa kukubali mwaliko wangu kwa mara nyingine kuwa mgeni rasmi na kuungana nasi katika siku hii adhimu kwa Mahakama na wadau wa sheria nchini.

**Mheshimiwa Rais**, maadhimisho ya siku ya sheria nchini hufanyika kila mwaka kuashiria kuanza kwa mwaka mpya wa kazi wa Mahakama. Maadhimisho haya hutanguliwa na wiki ya utoaji elimu kwa umma ambapo pamoja na shughuli nyingine, Mahakama hupata nafasi ya kuwasikiliza wananchi ambao hutoa mrejesho na maoni juu ya shughuli za utoaji haki nchini. Kwa mwaka huu wiki hiyo ilianza tarehe 22/01/2023 baada ya kufunguliwa na Mhe. Makamu wa Rais, **Dkt. Philip Isdor Mpango**. Utaratibu huu wa kuwasikiliza wananchi ni sehemu ya maboresho ya Mahakama katika utoaji na upatikanaji haki, unaomlenga mwananchi—*Citizen-Centric Justice Delivery*.

## 2. KAULI MBIU YA MWAKA 2023

Kila shauri linalosajiliwa katika ngazi husika ya Mahakama, lina taratibu zake na mtiririko wake kupitia hatua zilizoainishwa na sheria husika hadi Jaji au Hakimu atoe uamuzi (hukumu) kuhusiana na mgogoro huo. Majaji, Mahakimu na Mawakili hufuata hizi hatua na mitiririko hata pale ambapo zinasababisha shauri kuchukua miaka kadhaa mahakamani na hata gharama huongezeka kadri shauri linapopitia hizo hatua.

Usuluhishi ni aina ya utatuzi wa migogoro unaohimiza wahusika katika mgogoro kuzungumza na kutatua tofauti zao.

Kauli mbiu ya siku ya Sheria nchini mwaka huu ni "**UMUHIMU WA UTATUZI WA MIGOGORO KWA NJIA YA USULUHISHI KATIKA KUKUZA UCHUMI ENDELEVU: WAJIBU WA MAHAKAMA NA WADAU".**

**Mheshimiwa Rais**, nchi yetu kwa kuthamini na kutambua umuhimu wa usuluhishi imeifanya mbinu hii ya utatuzi wa migogoro kuwa sehemu ya Katiba yetu. Ibara ya 107A (2) (d) ya Katiba inaitaka Mahakama katika kutoa uamuzi wa mashauri, kuzingatia kukuza

na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro. Kanuni hii ya Katiba inazingatia faida kubwa za matumizi ya usuluhishi katika utatuzi wa migogoro zikijumuisha kupunguza gharama na muda wa kuendesha shauri na kuendeleza undugu miongoni mwa wadaawa. Faida hizi zina mchango mkubwa sana katika kukuza uchumi endelevu.

**Mheshimiwa Rais**, Ipo nukuu ya Jaji Warren E. Burger, aliyewahi kuwa Jaji Mkuu wa Marekani kati ya 1969 na 1986. Nukuu hii inayotajwa mara nyingi sana kama mfano, tunaweza kuitumia kufafanua malengo makubwa ya Kauli Mbiu ya Siku ya Sheria. Nukuu hii inasema:

> *"Watu wenye migogoro, kama walivyo watu wenye maumivu au magonjwa, wanapofika Mahakamani lengo lao kamwe sio kuwaona Majaji waliovaa majoho nadhifu au kuona vyumba vya Mahakama vilivyotiwa nakshi nzuri. Wanachotafuta ni NAFUU, na wanaitaka hiyo NAFUU kwa haraka na kwa gharama ndogo."*

Kauli Mbiu ya Mwaka huu (2023) inaitaka Mahakama, wadau wa Mahakama, wadaawa na wananchi kwa ujumla; tutatue migogoro kwa makubaliano au usuluhishi bila

kupoteza muda na gharama tukitumia ngazi na hatua ndefu za kimahakama hadi kusubiri hukumu.

*(a) Usuluhishi ni njia ya kutekeleza Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo*

**Mheshimiwa Rais**, Kauli Mbiu inalenga kuwasilisha ujumbe kuwa uchelewaji mkubwa wa mashauri ya madai na jinai Mahakamani unafifisha kasi ya kufikia Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo.

Dira yetu ya Taifa ya Maendeleo 2025 pamoja na mambo mengine inalenga kuwepo kwa **mazingira ya amani, usalama na umoja; utawala bora na utawala wa sheria; uwepo wa jamii iliyoelimika na inayojifunza**; na **kujenga uchumi imara na shindani**. Mahakama ya Tanzania inaamini kuwa, utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi ni kutekeleza Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya kuwawezesha wananchi wanaohusika na mashauri kutumia muda wao vizuri katika shughuli za kujenga uchumi.

*(b) Maelekezo ya Katiba kukuza na kuendeleza usuluhishi*

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) ambayo imeweka Kanuni mbili muhimu ambazo bado hazizingatiwi kikamilifu wakati wa kusikiliza mashauri Mahakamani na hivyo kusababisha uchelewaji mkubwa wa mashauri na kuongeza gharama za uendeshaji wa mashauri. Ibara ya 107A (2) (d) imetamka kanuni inayoitaka Mahakama, wakati inasikiliza mashauri ya madai au jinai, kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro. Ibara ya 107A (2) (e) imetamka kanuni nyingine muhimu sana kuwa, katika kutoa uamuzi wa mashauri ya madai na jinai kwa mujibu wa sheria, Mahakama zitende haki bila kufungwa kupita kiasi na masharti ya kiufundi yanayoweza kukwamisha haki kutendeka.

*(c) Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari limetunga sheria Kufanikisha Matumizi ya Usuluhishi*

Kauli Mbiu ya mwaka huu inakumbusha ukweli kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari limetunga sheria nyingi ambazo zinazofafanua utekelezaji wa Ibara ya 107A (2) (d) ya Katiba kuitaka Mahakama kukuza na kuendeleza usuluhishi.

**Mheshimiwa Rais**, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.1 ya mwaka 2020 *[Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act No. 1 of 2020]* iliyozifanyia marekebisho Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai (SURA YA 33) kwa kuongeza Kifungu kipya cha 64A, kinachotamka kuwa, wadaawa, sasa wana hiyari ya kutatua mgogoro wao nje ya Mahakama. Endapo wadaawa watafikia makubaliano nje ya Mahakama, watayasajili katika ngazi husika ya Mahakama na makubaliano hayo yatakuwa na nguvu ya amri ya mwisho ya Mahakama katika mgogoro huo. Ni wajibu wa Majaji, Mahakimu, Mawakili wa Serikali na Mawakili wa Kujitegemea; kila mara kuwakumbusha wadaawa uwepo wa hiyo nafasi ya kutatua migogoro nje ya Mahakama.

**Mheshimiwa Rais**, kwa nia hiyo hiyo ya kuwataka wenye migogoro kutumia usuluhishi badala ya kukimbilia Mahakamani, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheria ya Usuluhishi ya mwaka 2020 *(Arbitration Act, 2020)* ambayo, pamoja na mambo mengine, inaweka mfumo madhubuti wa usimamizi na uratibu wa wasuluhishi ikiwemo kuanzishwa kwa Kituo cha Usuluhishi Tanzania *(Tanzania Arbitration Centre)*.

Aidha, mwaka 2021 Wizara ya Katiba na Sheria ilitunga Kanuni mbalimbali (GN. 147, 148 na 149) zenye kutoa miongozo mbalimbali ya utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala. Hizi Kanuni ni pamoja na Uendeshaji wa Usuluhishi (Tangazo la Serikali Namba 146/2021); na Kanuni za Usajili wa Watakaofanya Kazi za Usuluhishi *(Arbitration)*, Upatanishi *(Mediation)*; Wasimamizi wa Majadiliano ya Kurudisha Mahusiano ya Kirafiki *(Reconciliation)* [Tangazo la Serikali Namba 146/2021]. Tunaipongeza Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuweka mazingira ya kisheria ya kusuluhisha migogoro nje ya Mahakama kwa kutoa orodha ya wasuluhishi.

*(d) Mihimili ya Bunge na Serikali Inatambua Usuluhishi ni Tiba ya Ucheleweshwaji wa Mashauri Mahakamani*

**Mheshimiwa Rais**, Kauli Mbiu ya Mwaka Huu inatoa tahadhari kwa Majaji, Mahakimu, Mawakili wa Serikali na Mawakili wa Kujitegemea ambao ndio wahusika wakubwa wa uendeshaji wa mashauri Mahakamani. Mihimili ya Bunge na Serikali, tayari imeelewa kuwa dawa ya ucheleweshwaji wa mashauri Mahakamani ni usuluhishi ambao tayari umewezeshwa kwa kutungiwa Sheria nyingi katika maeneo mbali mbali ambayo usuluhishi

unawezekana. Mhimili wa Mahakama na wadau wake, wataonekana kuwa wameshindwa mtihani wa viapo vyao na wajibu wao kulinda na kutetea Katiba na Sheria za nchi wasipotekeleza wajibu wao wa kufanikisha Usuluhishi. Tuchukue tahadhari, kuwa wananchi watatushtaki kwa waliotunga Sheria wakiona Haki inachelewa na sisi bado hatutumii Sheria zilizotungwa kutatua migogoro kwa njia ya Usuluhishi.

**Mheshimiwa Rais**, ushahidi upo kuwa Mihimili ya Bunge na Serikali ina ufahamu mkubwa kuhusu manufaa ya usuluhishi. Mhimili wa Mahakama na Wadau tutajiweka katika mazingira hatari mbele ya macho ya wananchi, endapo hatuzitumii Sheria zinazotoa nafasi za usuhishi na Sheria zinazotuzuia kutumia kanuni za kiufundi kuchelewesha haki. Mfano hapa ni Maoni ya **KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO** (07 Februari, 2020). Kupitia hayo maoni, Kamati hii ilitambua faida kubwa ya usuluhishi iliyosukuma kutungwa kwa Sheria ya Usuluhishi ya mwaka 2020. Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge (Sheria Ndogo) alitamka:

> "**Mheshimiwa Spika**, *Kabla sijazungumzia Maoni na Ushauri wa Kamati, naomba nieleze kwa ufupi kuhusu dhana ya Usuluhishi kwa muktadha wa mswada huu. Usuluhishi ni mfumo wa utatuzi wa migogoro hususan ya kibiashara kati ya pande*

*zilizo na mkataba kwa kusimamiwa na mtu au taasisi ambazo si mahakama lakini kwa kuzingatia taratibu zilizorahisishwa za kimahakama. Uamuzi unaotolewa katika Usuluhishi unaitwa tuzo za usuluhishi **(arbitral award)**. Usuluhishi unatajwa kuwa njia bora zaidi katika utatuzi wa migogoro kuliko mfumo wa kimahakama kwa kuwa mfumo huo:*

*a)-Unawezesha utatuzi wa migogoro kwa njia ambayo ni ya haraka, kirafiki na yenye ufanisi zaidi na hivyo kuchukuliwa kuwa unaboresha mazingira ya ufanyaji biashara;*

*b)-Unawezesha usiri **(confidentiality)** wa taarifa za wahusika kwa kuwa mfumo huu haufanyiki kwa uwazi **(no public hearing)**;*

*c)-Una uwezekano wa kupata watatuzi ambao wana utaalamu mahsusi katika eneo lenye mgogoro unaotatuliwa; na*

*d)-Taratibu za uendeshaji wa mashauri ya usuluhishi zinaweza kubadilishwa kuliko za mahakama **(flexibility)**."*

## 3. UMUHIMU WA UTATUZI WA MIGOGORO KWA NJIA YA USULUHISHI UNAFANANA NA FALSAFA YA MARIDHIANO, USTAHIMILIVU NA MABADILIKO YA KUJENGA UPYA NCHI

**Mheshimiwa Rais**, baada ya kuonyesha Kauli Mbiu inavyowakumbusha Mahakama na wadau wa Mahakama kuwa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi ni takwa la Kikatiba na Kisheria; sina budi kutambua na kuupongeza uongozi wako katika kukuza majadiliano na maridhiano katika siasa za Tanzania.

Ingawa Mahakama ya Tanzania katika Wiki na Siku ya Sheria ilichagua kauli mbiu ya kuhimiza USULUHISHI kama njia mbadala wa kutatua migogoro, wewe, Mhe. Rais, mapema mara baada ya kuingia madarakani tarehe 18 Machi, 2021 ulianza kuhimiza mazungumzo, majadiliano na usuluhishi kwenye migogoro ya kisiasa. Ulionyesha dhamira ya dhati ya kuleta maridhiano kwa kuunda kikosi kazi cha kukusanya maoni. Ulisema kwamba, busara zilikutuma, baada ya kuona haja ya kufanya Taifa liwe kitu kimoja, wote tuzungumze lugha moja; na ili Taifa liwe moja, uliendelea kusema, ni lazima kuwepo mazungumzo na maridhiano kwenye vyama vya siasa.

**Mheshimiwa Rais**, uliita juhudi zako kuwa falsafa ya kusimamia **maridhiano, ustahimilivu na mabadiliko ya kujenga upya nchi** katika Nyanja za siasa. Hapana shaka yoyote falsafa hiyo ndiyo iliyojengewa misingi elekezi kwa Mahakama chini ya Ibara ya 107A (2)(d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) inayoagiza Mahakama za Tanzania kutoa uamuzi wa mashauri ya madai na jinai kwa kuzingatia Sheria; na katika kuzingatia Sheria za Nchi, Mahakama zinatakiwa kufuata kanuni-elekezi ya kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro.

## 4. MAEENEO YALIYOONYESHA MAFANIKIO YA UTARATIBU WA USULUHISHI

### (i)- Kituo Cha Usuluhishi *(Mediation Centre)* cha Mahakama Kuu

*(a)-Faida za Usuluhishi*

Mheshimiwa Rais, uzoefu wa matumizi ya Usuhishi katika Kituo Cha Usuluhishi *(Mediation Centre)* cha Mahakama Kuu, unathibitisha usahihi wa Maoni ya KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO kuwa usuluhishi una faida nyingi.

**Mheshimiwa Rais**, kuanzishwa kwa Huduma ya Usuluhishi kama mbadala wa mashauri kusikilizwa mahakamani ni lengo muhimu sana katika Mpango Mkakati wa Mahakama na Programu ya Maboresho. Kimkakati na kimaboresho, Mahakama ya Tanzania iliona kuwa Usuluhishi ni mojawapo ya mikakati ya kuondoa ucheleweshwaji wa mashauri; kuwapunguzia majaji na mahakimu mizigo ya mashauri na kupunguza milundikano ya mashauri.

Katika kutekeleza azma hii ya Kimkakati na Kimaboresho kutumia taratibu za usuluhishi; mnamo mwaka 2015

Mahakama ya Tanzania ilianzisha KITUO CHA USULUHISHI katika ngazi ya Mahakama Kuu ili kujenga uzoefu na ufahamu wa kina kuhusu dhana ya Usuluhishi kisha kutumia uzoefu huo wa Usuluhishi kusaidia kurahisisha na kuharakisha utatuzi wa mashauri ya madai yanayofunguliwa, kwa kuanzia, katika Masjala za Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam na Divisheni ya Ardhi. Lengo la pili lilikuwa kutumia uzoefu uliopatikana kueneza matumizi ya usuluhishi katika ngazi zote za Mahakama nchini Tanzania.

**Mheshimiwa Rais**, kwa upande wa faida, takwimu za migogoro iliyosuluhishwa katika Kituo Cha Usuluhishi, yanaonyesha kuwa Wadaawa wameweza kutumia muda mfupi usiozidi siku thelathini **(30)** tangu walipofikia hatua ya usuluhishi kwa kuwa muda wa ukomo wa usuluhishi ni siku thelathini **30**. Tathmini ya uendeshaji wa usuluhishi wa mashauri haya inaonyesha upatanishi wa shauri moja umetumia muda wa saa **5** mpaka saa **21** hutumika na wadaawa katika kuongea, kujadili na kupata suluhu ya viini vya tatizo la migogoro hadi kufikia maridhiano.

Aidha, ukomo wa siku **30** wa kusuluhisha mgogoro ni muda mchache ukilinganisha na muda ambao wadaawa wenye mgogoro hutumia katika kukamilisha ngazi za

Mahakama na taratibu za kimahakama. Uzoefu katika Kituo cha Usuluhishi unaonyesha kiasi kikubwa cha fedha zinaokolewa kwa mashauri kukamilika kwa njia ya Usuluhishi. Wapo wadaawa ambao, baada ya kufikia maridhiano ya kutatua migogoro yao kwa usuluhishi, wameokoa kiasi kikubwa cha fedha ambazo zingelazimika kulipwa au wadaawa kufilisiwa mali zao ili kufidia madai endapo mashauri hayo yangeendelea katika hatua za kusikilizwa hadi kufikia hatua ya hukumu. Aidha, katika mashauri haya baadhi ya maridhiano yalihitaji tu hati za kuombana msamaha bila ya kuhusisha gharama za fedha zilizopo katika hati zao za madai.

**Mheshimiwa Rais**, Usuluhishi una faida kubwa katika mashauri kuhusu madai ya madeni ya mikopo ya benki. Hii ni kwa vile fedha zilizoshikiliwa kama dhamana huachiwa mapema baada ya usuluhishi badala ya kuendelea kushikiliwa kwa muda mrefu kusubiri hatua zote za hukumu na utekelezaaji wa hukumu.

Hivyo, kupitia uzoefu wa Kituo cha Usuluhishi, inaonekana wazi kabisa endapo taasisi za fedha na za kibenki zikitumia vyema njia hii ya upatanishi zinaweza kuokoa rasilimali na kuendeleza uchumi kwa kupitia dhamana ambazo zimekuwa zikishikiliwa na mabenki

na wakopaji kutokana na shauri kubaki mahakamani kwa muda mrefu. Hata hivyo, uzoefu wa Kituo cha Usuluhishi unaonyesha bado idadi kubwa ya mashauri haya yanayohusu mikopo yamekuwa na kiwango kidogo cha kufanikiwa katika hatua ya upatanishi hata pale mazingira ya upatanishi yanapokuwepo. Hii hutokana aidha na maafisa wanaowakilisha mabenki kutoichukulia hatua ya Usuluhishi kama fursa ya kutatua mgogoro; Au wanaowakilisha Mabenki kutokuwa na ruhusa ya kufanya majadiliano na kufikia usuluhishi bila kuomba ruhusa maalum kutoka kwa Bodi za Taasisi hizo.

*(b)-Ulinganifu baina ya Mashauri ya Usuluhishi na Mashauri Mengine ya Mabenki*

**Mheshimiwa Rais**, faida zinazotokana na Usuluhishi katika Kituo Cha Usuluhishi (Mahakama Kuu) huonekana vizuri pale ulinganifu unapofanywa na mashauri ya kibenki ambayo hayakupata nafasi ya kusuluhishwa.

Mfumo wa kutunza Maamuzi kwa Njia ya Mtandao *(TANZLII)* unaonyesha kuwa, kuanzia Januari hadi mwisho wa Desemba 2022, Mahakama ya Rufani ilisikiliza rufaa mbali mbali zipatazo **sitini (60)** zilizohusu Mabenki. Mashauri haya yanatoa picha, ya muda mrefu,

ambao mashauri yanayohusu mabenki na taasisi za kifedha, hutumia kuanzia kusajiliwa, kusikilizwa na kutolewa uamuzi na Mahakama Kuu, hadi kukatiwa rufaa, kusikilizwa na kutolewa maamuzi na Mahakama ya Rufani.

**SHAURI LA RUFANI YA MADAI NAMBA 511 LA MWAKA 2020 (CIVIL APPEAL NO. 511 OF 2020)** lilitokana na mgogoro wa kazi baina ya mtumishi wa benki na Benki (Mwajiri). Badala ya siku thelathini zinazotumika katika Kituo cha Usuluhishi, shauri lilichukua **MIAKA SABA** kuanzia mtumishi aliposimamishwa kazi hadi uamuzi wa Mahakama ya Rufani ulipotolewa. Baada ya Uamuzi wa Mahakama Kuu, mtumishi alisubiri **MIAKA MITANO** hadi Mahakama ya Rufani iliposikiliza rufaa iliyowasilishwa na Benki na Mahakama ya Rufani kuitupilia mbali rufaa hiyo. Miaka saba ni mingi sana kupotea ikizingatiwa kuwa uzoefu katika Kituo cha Usuluhishi muda wa ukomo wa usuluhishi ni siku **30 tu.**

**Mheshimiwa Rais**, mfano mwingine ni **RUFANI YA MADAI NAMBA 374 YA MWAKA 2019 (CIVIL APPEAL NO. 374 OF 2019)** iliyosikilizwa na Mahakama ya Rufani na ilitokana na mkopo wa mwaka **2010** wa shilingi **541,031,841.70** kwa ajili ya kununua **excavator**

na **greda**. Ingawa hadi kufikia mwaka 2013, mkopaji alikuwa amelipa kiasi kikubwa cha deni, alishindwa kulipa kwa wakati miamala ya malipo yaliyobaki. Benki ikachukua hatua ya kumnyangánya mteja **excavator** na **greda** kisha kuiuza kwa mtu mwingine. Mteja akafungua shauri Mahakama Kuu na wakati huo huo Benki ikafungua katika shauri hilo hilo **MADAI-KINZANI *(COUNTER-CLAIM)***. Katika uamuzi wake, Mahakama Kuu ikaamua kuwa Benki haikuwa na haki ya kunyangánya mteja wake **excavator** na **greda** na kuviuza.

Benki hawakuridhika na walikata rufaa katika Mahakama ya Rufani. Mahakama ya Rufani ilitengua uamuzi wa Mahakama Kuu kwa sababu iliona Mahakama Kuu ilikosea kwa kushindwa kutoa uamuzi wake juu ya Madai-Kinzani ya Benki *(Counter-Claim)*. Mahakama ya Rufani ikalirudisha shauri Mahakama Kuu ili ikatayarishe hukumu nyingine upya itakayozingatia pia Madai-Kinzani. Hapa picha ya ucheleweshwaji inaonekana pale, Uamuzi wa awali wa Mahakama Kuu ulitolewa tarehe **19/08/2016**. Ilichukua **MIAKA SITA** baadaye hadi Mahakama ya Rufani iliposikiliza rufani na kutoa uamuzi tarehe **11/03/2022** wa kurudisha Mahakama Kuu itoe hukumu inayozingatia Madai-Kinzani. Baada

ya Mahakama Kuu kurudishiwa shauri, kutakuwa na ucheleweshwaji kwa vile, endapo baada ya Mahakama Kuu kuandika hukumu upya, na yeyote hataridhika na huo uamuzi mpya; utaratibu wa kukata rufani kurudi Mahakama ya rufani utafuata.

*(c)-Ulinganifu baina ya Mashauri ya Usuluhishi na Mashauri ya Kodi*

**Mheshimiwa Rais**, baada ya kuona kuwa Kituo Cha Usuhishi kinamaliza mashauri kwa Usuluhishi ndani ya Siku thelathini, hali ni tofauti kwa mashauri kuhusu migogoro ya kodi yanayopitia ngazi tatu za rufaa za kodi. Ngazi ya mwanzo kabisa ni Bodi ya Rufaa za Kodi *(Tax Revenue Appeals Board—TRAB)*. Ngazi ya Pili ni Baraza la Rufaa za Kodi *(Tax Revenue Appeals Tribunal—TRAT)*. Ngazi ya tatu na ya mwisho, ni Mahakama ya Rufani *(Court of Appeal of Tanzania)*.

Hapana shaka yoyote kuwa, Usuluhishi na Upatanishi katika migogoro ya Kodi, una faida kubwa kwa uchumi. Ukweli huu unaonekana ukilinganisha uzoefu wa Kituo cha Usuluhishi kukamilisha Usuluhishi ndani ya Siku thelathini, na miaka kadhaa ambayo husubiriwa mashauri ya Kodi yakamilishe safari kupitia ngazi tatu ambazo

mashauri kuhusu migogoro ya kodi hulazimika kupitia.

Kati Januari na Desemba 2022, Mahakama ya Rufani ilipandisha jumla ya maamuzi **1,205** katika Mtandao wake wa TANZLII. Kati ya hayo kulikuwa na takriban Rufaa au Maombi **13** ambayo yalikuwa rufaa za kodi zilizoihusisha Mamlaka ya Mapato Tanzania kama mrufani au mrufaniwa.

**Mheshimiwa Rais**, Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Mapato alikuwa ni Mrufani katika **RUFANI YA MADAI NAMBA 11 YA 2020 (CIVIL APPEAL NO. 11 OF 2020)** dhidi ya KAMPUNI KUBWA ya uchimbaji dhahabu. Uamuzi wa Bodi ya Rufani za Kodi katika ngazi ya kwanza ya rufani ulifanyika Mwaka 2010. Ngazi ya pili ya uamuzi wa Baraza la Rufani za Kodi ulifanyika miaka miwili baadaye tarehe 1/10/2012. Mahakama ya Rufani Tanzania ilisikiliza na kutoa uamuzi wa mwisho katika ngazi ya tatu tarehe 17/03/2022 yaani uchelewaji kwa miaka **12** baada ya uamuzi wa Bodi, na miaka **10** baada ya uamuzi wa Baraza la Rufani za Kodi. Hii ina maana kuwa, endapo Usuluhishi ungefanyika mgogoro ungekamilika ndani ya mwezi mmoja badala ya kusubiri miaka **12**.

**RUFANI YA MADAI NAMBA 444 YA 2020 (CIVIL APPEAL NO. 444 OF 2020)** ni mfano mwingine muda mrefu unaopotea katika mashauri ya kodi na kwa gharama kubwa. Hii Rufaa Namba 444/2020 ilikuwa baina ya Kampuni ya Sukari dhidi ya Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Mapato. Mgogoro wa kodi uliwasilishwa ngazi ya kwanza, mbele ya Bodi ya Rufaa za Kodi, mwaka 2017. Uamuzi wa Baraza la Rufaa za Kodi kama ngazi ya pili, ulitolewa miaka mitatu baadaye mnamo tarehe 16/09/2020. Uamuzi wa Mahakama ya Rufani ambayo ndio ngazi ya tatu na ya mwisho katika rufani za kodi ulisomwa tarehe 30/05/2022 ikiwa takriban **miaka MITANO** tangu mgogoro ulipowasilishwa mbele ya Bodi ya Rufaa za Kodi.

**Mheshimiwa Rais**, mfano mwingine ni **RUFANI YA MADAI NAMBA 192 YA 2021 (CIVIL APPEAL NO. 11 OF 2020).** Mgogoro ulianza kusikilizwa na kuamuliwa na Bodi ya Rufaa ya Kodi mwaka 2017, miaka mitatu baadaye Baraza la Rufani za Kodi lilitoa uamuzi wake tarehe 16/11/2020. Uamuzi wa Mahakama ya Rufani ulitolewa tarehe 22/09/2022 hii ni **miaka mitano** baada ya shauri kuwasilishwa katika ngazi ya Bodi.

**Mheshimiwa Rais**, kwa bahati nzuri, Bunge lilitambua umuhimu wa usuluhishi kwenye migogoro ya Kodi na kufanya marekebisho ya Sheria. Sheria ya Rufani za Kodi SURA YA 408 *[Revenue Appeals Act Cap. 408]* ilifanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Fedha Namba 3 ya Mwaka 2021. Sheria ya Fedha Namba 3 ya Mwaka 2021 iliongeza vifungu vidogo vya (6) na (7) katika Kifungu cha 22 cha Sheria ya Rufani za Kodi ili kuwaruhusu wadaawa katika migogoro ya kodi kuomba muda wa kuzungumza na kufikia makubaliano na kutoa taarifa ya makubaliano yao ndani ya muda utakaotajwa na Bodi ya Rufani za Kodi au na Baraza la Rufani za Kodi. Ni dhahiri baada ya marekebisho hayo ya sheria, migogoro ya kodi itatumia muda mfupi zaidi katika ngazi za rufaa za kodi endapo wahusika watatumia utaratibu wa UPATANISHI *(Mediation)* na kufikia Usuluhishi.

Hapana ubishi kuwa ucheleweshwaji wa mashauri ya madai au ya jinai, yana gharama kubwa kwa uchumi wa nchi yoyote. Mara nyingi wakati mashauri yanapokuwa katika mlolongo wa ngazi na taratibu ndefu za kimahakama, matumizi ya mali husika na mgogoro, au fedha, au hata ardhi inayohusika na mgogoro; husimama kuisubiri ngazi husika ya Mahakama kukamilisha usikilizaji wa mgogoro,

na mara nyingi migogoro hupitia ngazi zote za Mahakama husubiri hadi kusubiri uamuzi wa Mahakama ya Rufani.

*(d)-Ulinganifu baina Mashauri ya Usuluhishi na Mashauri ya Kawaida yenye Mitiririko na Vituo Vingi Vinavyoongeza Ucheleweshwaji na Gharama*

**Mheshimiwa Rais**, tumeona ngazi tatu za Mahakama ambazo migogoro ya kodi hupitia kwa wastani wa sio chini ya miaka mitano. Moja ya faida kubwa ya Usuluhishi ni wadaawa kuepuka ngazi hizo tatu au nne za Mahakama ambazo mashauri hupitia, na kila ngazi kuwa na taratibu zenye mizunguko mingi ambazo huongeza gharama na kuchangia kuchelewesha mashauri kukamilika.

**Mheshimiwa Rais**, Mgogoro baina ya RUFAA NAMBA 45 YA MWAKA 2015 (CIVIL APPEAL NO 45 OF 2015), FELICIAN FERDINAND na SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO) ni mfano wa mgogoro kuhusu jambo dogo kuhusu kusitishwa kwa huduma za umeme. Mgogoro huu mdogo ulioanza mwaka 2002, ukazunguka ngazi tatu za Mahakama na kudumu Mahakamani kwa zaidi ya miaka 15 hadi kufika mbele ya jopo la Majaji wa Mahakama ya Rufani katika ngazi ya TATU tarehe 9/10/2018 na kusubirishwa ili kumpata msimamizi wa mirathi.

Mgogoro ulianza tarehe 15 Mei, 2002 wakati mafundi wa SHIRIKA LA UMEME walipositisha huduma ya umeme kuendesha mashine ya kusaga unga, *Nyakato Posho Mill*, iliyokuwa inamilikiwa na Felician Ferdinand. Siku mbili baadaye (17/5/2002), mfanya biashara huyu aliyekuwa jijini Mwanza alifungua shauri katika Mahakama ya Wilaya Mwanza akielezea namna TANESCO Mwanza, bila taarifa ya awali, walivyositisha huduma ya umeme katika mashine yake ya kusaga unga iliyokuwa ikimuingizia kipato cha SHILINGI ELFU SITINI kila siku. Wakati huduma ya umeme inasitishwa alikuwa amepokea kile alichokiita, "tenda kubwa" kutoka Nakuru-Kenya ya kutayarisha tani 395 ya unga wenye thamani ya shilingi milioni kumi kutokana na Samaki wanaotayarishwa kama chakula cha kuku.

**Mheshimiwa Rais**, Shauri hili lilichukua muda mrefu Mahakama ya Wilaya kutokana na maahirisho mengi kutokana na sababu mbali mbali za kiufundi au wadaawa kutofika Mahakamani. Takriban miaka minne baada ya Felician Ferdinand kufungua shauri, tarehe 07/02/2006 TANESCO walishindwa kutokea Mahakamani na Mahakama ya Wilaya ikaamuru shauri lisikilizwe upande mmoja kwa njia ya Hati ya Viapo. Tarehe 10/03/2006

Mahakama ya Wilaya ilisoma hukumu ya upande mmoja bila kuwasikiliza TANESCO na hukumu hiyo ilimpa ushindi Felician Ferdinand.

Miezi minane baada ya hukumu ya upande mmoja kusomwa, TANESCO walizinduka na wakaleta Hati ya Kiapo kuiomba Mahakama ya Wilaya itengue hukumu ya upande mmoja. Mahakama ya Wilaya ilikubali na kutoa amri kuwa kesi isikilizwe upya ikiwa na uwakilishi wa TANESCO. Mahakama ya Wilaya Nyamagana ilisikiliza kesi hii kwa muda wa miaka minne hadi tarehe 6/12/2010 iliposoma hukumu iliyotoa ushindi kwa Felician Ferdinand. Mahakama iliamuru TANESCO imlipe Felician Ferdinand fidia ya shilingi Tshs. 9,875,000/=. Iliamuru Ferdinand alipwe shilingi laki tatu na nusu kama fidia ya kupoteza mapato kila siku kuanzia tarehe ambayo TANESCO walisitisha huduma ya umeme. Mahakama iliamuru TANESCO wamlipe Ferdinand shilingi milioni kumi kama fidia kwa maumivu mbali mbali aliyoyapata.

TANESCO hawakuridhika na uamuzi wa Mahakama ya Wilaya na tarehe 26/01/2011 waliwasilisha Hati ya Rufani Mahakama Kuu Mwanza. Jaji wa Mahakama alisoma hukumu yake tarehe 28/07/2011 (hii ni **miaka 9** baada ya Felician Ferdinand kukatiwa umeme na

TANESCO). Jaji alithibitisha uamuzi wa Mahakama ya Wilaya kuwa TANESCO hawakuwa sahihi walipokata huduma za umeme na akaamuru TANESCO wamlipe Felician Ferdinand **shilingi milioni kumi**. Hata hivyo, Jaji wa Mahakama Kuu alitengua amri ya Mahakama ya Wilaya kuamuru TANESCO imlipe Ferdinand fidia ya shilingi 350,000 ya kukosa mapato ya kila siku.

FELICIAN FERDINAND hakuridhika na uamuzi wa Mahakama Kuu kuwa alipwe shilingi milioni kumi tu. Akaanza safari ndefu na milolongo ya kuwasilisha rufani yake Mahakama ya Rufani. Tarehe 08/10/2012 (**miaka kumi** baada ya kukatiwa umeme) aliwasilisha Taarifa ya Nia ya Kukata Rufani *(Notice of Appeal)* na akaomba atayarishiwe na kupewa nakala ya kumbukumbu za mwenendo wa shauri lake na maamuzi yote ya Mahakama za chini.

Na kwa kuwa mgogoro wake na TANESCO ulianzia katika Mahakama ya Wilaya, Sheria inayosimamia Uendeshaji wa Mashauri ya Mahakama ya Rufani ilimtaka Felician Ferdinand apate ruhusa *(leave)* ya Mahakama Kuu kabla ya kuwasilisha rufaa katika Mahakama ya Rufani.

Hivyo basi, tarehe 08/10/2012, Felician Ferdinand aliwasilisha ombi Mahakama Kuu apewe hiyo ruhusa *(leave to appeal to the Court of Appeal)* ya kukata rufani Mahakama ya Rufani. Ombi hili halikusikilizwa mara moja. Takriban miezi saba ilipita hadi tarehe 18/06/2013 tangu Ferdinand awasilishe ombi la ruhusa, TANESCO waliwasilisha Hati ya Kiapo-Kinzani *(Counter Affidavit)* kupinga ombi la FERDINAND kuruhusiwa kukata rufaa katika Mahakama ya Rufani. TANESCO waliwasilisha pia pingamizi la kisheria kuwa Hati ya Kiapo aliyowasilisha Ferdinand ilikuwa na mapungufu ya kisheria na iondolewe akalete nyingine.

**Mheshimiwa Rais**, Mifumo yetu ya utoaji haki ina mitiririko na kona kona na vituo vidogo vidogo vingi mno. Mfumo una vizuizi vingi, na hatua nyingi ambazo hazina mantiki zaidi ya kuchangia ucheleweshwaji wa usikilizwaji wa misingi ya migogoro. Kwa mfano, tarehe 28/05/2013 Jaji wa Mahakama Kuu Mwanza alikuwa tayari kusikiliza Ombi la Ferdinand la ruhusa ya kukata rufani Mahakama ya Rufani. Mawakili hawakuwa tayari. Wakamwambia Jaji: *"We are still corresponding with our clients who have not yet formally instructed us. To that effect we pray for more time to file counter affidavit."* Jaji aliahirisha

shauri kwa miezi miwili hadi tarehe 13/08/2013.

Tarehe 13/08/2013 ilipofika Shauri liliahirishwa mara kadhaa kwa sababu mbali mbali hadi iliposikilizwa tarehe 01/04/2014 na uamuzi wa kumruhusu Felician Ferdinand akate rufaa yake ulisomwa tarehe 03/06/2014 **(miezi miwili baada ya Jaji kusikiliza)**.

Pamoja na kuruhusiwa kukata rufani, Felician Ferdinand ilibidi tarehe 28/07/2014 amuandikie barua Naibu Msajili wa Mahakama Kuu Mwanza kumkumbusha ampe kumbukumbu za mwenendo wa mashauri ili atayarishe Kitabu cha Rufani *(record of appeal)*. Baada ya barua hii, Ferdinand alisubiri kwa takriban miezi **MITANO** hadi tarehe 14/01/2015 alipoitwa kwenda kuchukua kumbukumbu na mwenendo mzima. Ferdinand aliwasilisha rufaa yake na ikapewa Namba 45 ya 2015, hii ilikuwa **miaka 13** baada ya kukatiwa umeme.

Mheshimiwa Rais, Kuwasilisha rufaa katika Mahakama ya Rufani na kupewa Namba ya Rufaa, ni hatua ya mwanzo tu kabla ya rufani kusikilizwa. Ilikuwa tarehe 13/12/2017 (miaka miwili baada ya kuwasilisha rufaa na miaka 15 baada ya kukatiwa umeme) ndipo Ferdinand alipoitwa kusikilizwa na Mahakama ya Rufani. Felician Ferdinand

hakuweza kufika Mahakamani. Alifika ndugu yake Philimon Felician Minde; ambaye aliijulisha Mahakama ya Rufani kuwa Felician Ferdinand alikuwa tayari amefariki. Mahakama ya Rufani ikaahirisha usikilizwaji wa Rufaa kusubiri familia ya marehemu Felician Ferdinand imteue Msimamizi wa Mirathi ya FELICIAN FERDINAND ili aje asimamie rufani kwa niaba ya marehemu.

**Mheshimiwa Rais**, Niseme Mgogoro baina ya FELICIAN FERDINAND na TANESCO ni mgogoro ambao ungemalizika ndani muda mfupi kama pande husika zingeanza kwa kutafuta usuluhishi.

### (ii)- Umuhimu wa Usuluhishi katika Utatuzi wa Migogoro ya Kazi

**Mheshimiwa Rais**, Taarifa ya Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi kwa Mwaka 2022 inakiri kuwa Sheria inayolazimu migogoro ya kazi ianzie kwa njia ya usuluhishi imesaidia sana kupunguza milundikano ya migogoro hiyo katika hatua ya Mahakama Kuu.

Kifungu cha 86(4) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini kimeelekeza kwa ulazima mgogoro kuhusu kazi/ajira uanzie katika hatua ya usuluhishi. Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) ni Tume huru iliyoanzishwa chini

ya kifungu cha 12 cha Sheria ya Taasisi za Kazi Sura ya 300. Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ilianzishwa ili kutekeleza majukumu makubwa mawili, la kwanza likiwa ni kusuluhisha migogoro ya kikazi na, pili; kuamua migogoro ya kikazi pale usuluhishi unaposhindikana.

Kama zilivyo taasisi nyingine za kazi ikiwemo Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) ilianzishwa kufuatia mabadiliko makubwa ya sheria za kazi nchini yaliyofanyika mwaka 2004 kwa kufuta sheria za kazi za zamani na badala yake kutungwa kwa **Sheria ya Taasisi za Kazi (Sura ya 300)** na **Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini (Sura ya 366)**.

Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini imesisitiza kuwa utatuzi wa mgogoro katika hatua ya usuluhishi, usizidi muda wa siku **30**. Jambo zuri na la kupongezwa ni kwamba uzoefu kupitia taarifa za Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) unaonesha kuwa mashauri huisha kati ya siku **7** hadi **21** tangu kufunguliwa na kufikishwa mbele ya msuluhishi. Uharakishwaji huo huwafanya wadaawa wasitumie muda mrefu kwenye mashauri ili muda mwingi utumike kwenye shughuli za uzalishaji zinazokuza uchumi.

*(a)-Faida ya Usuluhishi katika Migogoro ya Kazi*

**Mheshimiwa Rais**, faida ya matumizi ya usuluhishi kupitia Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) unaonekana katika maeneo kadhaa. **Kwanza,** kuchochea maendeleo ya uchumi na kuongeza uzalishaji. Kuna uhusiano mkubwa sana wa majukumu ya Tume hasa usuluhishi wa migogoro na ukuaji wa uchumi. Hii ni kwa sababu wadaawa wanaowasilisha mashauri mbele ya Tume ni waajiri na waajiriwa ambao ndiyo wahusika wakuu wa uzalishaji katika Serikali, viwanda, makampuni mbalimbali na watu binafsi. Hivyo basi kuwepo migogoro isiyokwisha kunaweza kwa kiasi kikubwa kuzorotesha uzalishaji na kupunguza ufanisi na hatimae kuzorotesha ukuaji wa uchumi. Kuna migogoro mikubwa inayoweza kuathiri moja kwa moja uzalishaji kwa mfano migomo viwandani *(industrial actions)*, kufungiwa nje kwa wafanyakazi *(lock-outs)* na kadhalika. Migogoro huu hugusa sehemu kubwa ya uzalishaji katika sekta husika na kuleta mtikisiko wa uchumi ambao huweza kuonekana moja kwa moja kwenye jamii mfano kuleta upungufu wa bidhaa katika soko au ongezeko (mfumuko) wa bei na hata upungufu kwenye ukusanyaji wa kodi. Hivyo basi ni vyema migogoro hii kusuluhishwa kwa haraka ili kuwafanya wahusika warudi kujikita katika uzalishaji kwa maendeleo endelevu ya uchumi wetu.

**Mheshimiwa Rais**, eneo la **PILI** la umuhimu wa matumizi ya usuluhishi kupitia Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) ni Kuvutia wawekezaji wa nje na wa ndani. Wawekezaji huvutiwa na mazingira ya uwekezaji ambayo hawatatumia gharama kubwa kuendesha mashauri pindi migogoro ya kikazi inapotokea. Wawekezaji huvutiwa pia na mazingira ambayo muda mfupi unatumika kutatua migogoro na hivyo kutoathiri kwa kiwango kikubwa, kasi na wingi wa uzalishaji. Ikumbukwe kwamba kiuchumi muda ni mali na ukipotea huleta madhara makubwa katika ukuaji wa uzalishaji na uchumi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Rais**, eneo la **TATU** la umuhimu wa matumizi ya usuluhishi kupitia Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) ni Tume hii kutoa huduma za usuluhishi na uamuzi wa migogoro ya kikazi bure, bila malipo. Hii ina maana kuwa, wadaawa ambao ni waajiri na wafanyakazi hawaingii gharama zozote mbele ya Tume kuanzia kufunguliwa kwa mgogoro hadi mwisho. Hii ni tofauti na vyombo vingine vya haki ambapo wadaawa hulazimika kulipia gharama mbalimbali ikiwemo gharama za kufungua shauri, kukazia deni tuzo na maombi mbalimbali. Kiuchumi usuluhishi na uamuzi wa migogoro unapokuwa bure inamfanya mtu yeyote hata asiyejiweza

kifedha apate haki yake, hivyo basi waajiri hupendelea zaidi kumaliza migogoro katika ngazi ya mahala pa kazi. Hali hii inachangia ukuaji wa uchumi kwa kuondoa ama kupunguza gharama za uendeshaji mashauri.

**Mheshimiwa Rais**, eneo la **NNE** la umuhimu wa matumizi ya usuluhishi kupitia Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) ni ukweli kuwa Tume inatekeleza kwa vitendo Ibara ya 107A (2) (e) ya Katiba ya Tanzania (1977) inayoelekeza Mahakama, kutenda haki bila kufungwa kupita kiasi na masharti ya kiufundi yanayoweza kukwamisha haki kutendeka. Kifungu cha 88(4) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini kimesisitiza kwamba katika usikilizaji wa mashauri, Tume inapaswa kusikiliza migogoro kwa haraka na kwa haki pasipo kufungwa na mambo ya kiufundi. Njia na taratibu za utatuzi wa migogoro katika Tume ni rahisi na rafiki kwa kila mtanzania. Kwa kuongezea katika hili, wadaawa hawalazimiki kuajiri wawakilishi maana wana uwezo wa kujiwakilisha wenyewe kwa kuwa masuala ya kiufundi sio kipaumbele.

*(b) Uwezekano Mkubwa wa Usuluhishi wa Migogoro ya Kazi Kwa Mtandao*

**Mheshimiwa Rais**, wakati Mahakama ya Tanzania inajiondoa kwenye matumizi ya karatasi na kuingia katika matumizi ya TEHAMA kuanzia usajili, usikilizwaji na utolewaji wa maamuzi, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) inajikongoja. Hivi karibuni Tume imeanza mchakato wa kuingia kidijitali ili kuendana na kasi ya ukuaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) duniani ikiwemo usajili wa migogoro kwa njia ya mtandao. Hili ni jambo la kupongeza lakini hata hivyo kutokana na ufinyu wa bajeti, safari hii itakuwa ndefu ilhali kasi ya Karne ya 21 ni kubwa mno. Hivyo basi tunaiomba Wizara inayosimamia Tume hii, iisaidie kuharakisha mchakato huo ili kuenda na kasi na viwango vya Mahakama kwenye utoaji haki nchini. Kwa sasa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi wameanzisha utaratibu wa kufungua mashauri kwa njia ya ki-elektroniki ingawa ndio kwanza unaanza na matumizi yake bado hayajawa makubwa.

**Mheshimiwa Rais**, ufanisi utaongezeka zaidi iwapo itafika siku Tume itafanya usuluhishi kwa njia ya mtandao *(video comference)* bila ya kumlazimu muajiri kuacha ofisi na kwenda kwenye usuluhishi. Kwa kuwa makampuni mengi yana uongozi na ngazi za maamuzi sehemu mbalimbali

ndani na nje ya nchi, matumizi ya TEHAMA yatasaidia usuluhishi kuwa wa haraka kwa kuweza kumfikia mtoa maamuzi wa kampuni pahali alipo na akawa sehemu ya usuluhishi.

**Mheshimiwa Rais**, kwa upande wa Mahakama, tumeiagiza Idara ya TEHAMA ya Mahakama, kuunganisha *(link)* Mfumo wa Divisheni ya Kazi wa MENEJIMENTI YA MASHAURI KWA NJIA YA MTANDAO *(E-Case Management System)* ili upokee mashauri yanayotoka Tume ya Usuluhishi na Uamuzi. Kuunganishwa huku kuna umuhimu mkubwa kwa sababu asilimia zaidi ya **80%** ya mashauri yaliyopo katika Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi yanatokana na maamuzi ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi.

# 5. MAENEO MUHIMU YA KIUCHUMI NA KIJAMII YANAYOHITAJI USULUHISHI

## a. Usuluhishi katika kutatua Migogoro ya Ardhi

**Mheshimiwa Rais**, sina haja ya kuelezea umuhimu wa ardhi kwa uchumi wa nchi na kwa mwananchi mmoja mmoja. Migogoro ya ardhi isiyokuwa na mifumo thabiti ya utatuzi, ni adui mkubwa wa maendeleo, amani na ustawi wa wananchi.

Sheria ya Mahakama za Ardhi, Sura ya 216 *(Land Disputes Courts Act Cap. 216)* inatambua umuhimu wa matumizi ya Usuluhishi katika kutatua migogoro ya ardhi inayofikishwa mbele ya Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji *(Village Land Councils)* na kwenye Mabaraza ya Kata *(Ward Tribunals)*. Kifungu cha 8 cha Sheria ya Mahakama za Ardhi kimetamka kuwa moja ya majukumu ya Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji ni usuluhishi wa migogoro ya ardhi ndani ya maeneo ya Kijiji husika. Kwa upande mwingine, Kifungu cha 13 (4) cha Sheria ya Mahakama za Ardhi kimeyaagiza Mabaraza ya Kata, kufanya jitihada za kutumia usuluhishi kutatua migogoro ya ardhi na ikiwezekana hata kuahirisha usikilizaji kama wahusika wanataka nafasi ya kutafuta usuluhisho.

**Mheshimiwa Rais**, katika Taarifa yake ya Mashauri ya Ardhi ya mwaka 2022, Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi imeonyesha namna pale ambapo Mazungumzo, Majadiliano na Usuluhishi yametumika, na kusaidia kupunguza milundikano ya mashauri na kuharakisha usikilizwaji wa mashauri ya ardhi. Kwa mwaka 2022 Divisheni Ardhi ilisajili mashauri ya Ardhi yapatayo **elfu mbili mia moja na kumi na moja** (**2,111**) na pia ilisikiliza na kuamua mashauri yapatayo elfu mbili na mia saba na sitini na nane **(2,768**). Hadi kufikia Desemba 31, 2022 Divisheni ilikuwa imebaki na jumla ya mashauri yapatayo mia tisa na thelathini na tano **(935)**. Idadi ya mashauri yaliyobaki mwaka 2022 imepungua kutoka mashauri **1,591** yaliyobaki mwaka 2021 sawa na punguzo la **asilimia 58.**7.

Mafanikio ya Divisheni ya Ardhi ya kupunguza mashauri yanayobaki mwishoni mwa mwaka 2022, ni matokeo ya hatua mbalimbali zilizochukuliwa ikiwemo ya MAZUNGUMZO baina ya Divisheni na Ofisi ya Msajili wa Hati katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mazungumzo na Majadiliano haya yalihusu kifungu cha 99 cha Sheria ya Usajili wa Ardhi, Sura ya 334. Kifungu hiki kinaipa Mahakama Kuu pamoja na Ofisi ya

Msajili wa Hati mamlaka sawa (*concurrent jurisdiction*) katika kutatua migogoro inayohusu ardhi zenye usajili wa Hati (milki za ardhi zilizosajiliwa).

Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi na Ofisi ya Msajili wa Hati walijadiliana na kukubaliana hatua bora ya kupunguza wadaawa kukimbilia Mahakamani kuhusu migogoro ya ardhi zenye usajili wa Hati (milki za ardhi zilizosajiliwa). Walikubaliana kuwa migogoro inayohusu ardhi zenye usajili ziwasilishwe na kusikilizwa kwanza na Msajili wa Hati. Kifungu cha 102 cha Sheria ya Usajili wa Ardhi kinatoa nafasi kwa mdaawa ambaye amesikilizwa na Msajili wa Hati na hakuridhika na uamuzi, ndio akate rufaa kwenda Mahakama Kuu.

Majadiliano yaliyofanyika Mwezi June, 2022 kati ya Ofisi ya Msajili wa Hati na Mahakama Kuu - Divisheni ya Ardhi yalitambua ukweli kuwa, Msajili wa Hati ndiye mtunzaji *(custodian)* wa taarifa zote zinazohusu ardhi iliyopimwa na kusajiliwa hivyo yeye ndiye mwenye nafasi bora zaidi ya Mahakama kutatua katika hatua za awali migogoro yote inayotokana na ardhi zilizosajiliwa. Aidha, Utaratibu huu umewawezesha na kuwarahisishia wadaawa kushughulikia migogoro yao ya ardhi kwa haraka mbele ya Msajili wa Hati. Halikadhalika, imeongeza wigo wa rufaa

kwa mdaawa asiyeridhika na maamuzi ya Msajili wa Hati atakuwa na nafasi ya kukata rufaa mbele ya Mahakama Kuu na asiporidhika na uamuzi wa Mahakama Kuu akate rufaa Mahakama ya Rufani.

**Mheshimiwa Rais**, majadiliano baina ya Msajili wa Hati na Divisheni ya Ardhi ni mfano wa kuigwa na taasisi zote katika mnyororo wa utoaji haki, kuwa zinaweza kujadiliana na kukubaliana namna bora ya kutekeleza sheria na taratibu za Kimahakama zinazoongoza utatuzi wa migogoro.

**Mheshimiwa Rais**, Taarifa ya Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi inaonyesha namna Divisheni ilivyoweza kutumia Kituo cha Usuluhishi na Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi kutatua migogoro ya ardhi kwa njia ya usuluhishi. Kwa mwaka 2022, Mahakama Kuu-Divisheni ya Ardhi iliwasilisha jumla ya mashauri yapatayo mia mbili na kumi na sita **(216)** katika kituo cha Usuluhishi kwa ajili usuluhishi katika Kituo hicho. Mashauri ishirini na saba **(27)** kati ya mashauri 216), Usuluhishi ulifanikiwa kwa 100%. Mashauri **5** kati ya 216 Usuluhishi ulifanikiwa kwa kiasi **(partly)**. Mashauri **184** usuluhishi wake haukufanikiwa.

**Mheshimiwa Rais**, Taarifa inatoa sababu za kutofanikisha usuluhishi. Usuluhishi haukufanikiwa kwa asilimia kubwa kwasababu ya wadaawa kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusiana na faida za usuluhishi. Aidha, muda uliopangwa kisheria wa mwezi mmoja wa kukamilisha usuluhishi ulikuwa ni mdogo. Sababu nyingine ya kutofanikiwa kwa usuluhishi ni kwamba, baadhi ya Mawakili hupendelea zaidi usikilizwaji wa kawaida wa mashauri na mapambano ya kisheria mahakamani *(adversarial litigation)* kuliko usuluhishi.

### (b) Umuhimu wa Usuluhishi katika kutatua Migogoro ya Taasisi za Kidini

**Mheshimiwa Rais**, Usuluhishi, na kutokimbilia mahakamani; ni muhimu sana katika taasisi za dini. Viongozi wa dini wana mchango mkubwa katika kutatua migogoro ya waumini wao kwa njia ya usuluhishi. Migogoro mingi ya wananchi haifikishwi Mahakamani kwa sababu husuluhishwa na viongozi wa dini na madhehebu mbali mbali. Kwa bahati mbaya, ipo migogoro ndani ya taasisi za kidini, Makanisa, Misikiti, Mabaraza ya Wadhamini wa Taasisi za Kidini ambazo huwasilishwa Mahakamani badala ya kutafutiwa suluhisho ndani ya taasisi za kidini husika. Migogoro hii inahusu mali,

uongozi, na hata uchaguzi ndani ya Taasisi husika.

**Mheshimiwa Rais**, Mahakama Kuu ya Tanzania imewahi kuelekeza kuwa taasisi za kidini hazistahili kupeleka migogoro ya ndani ya taasisi zao moja kwa moja mahakamani, bila kwanza kupitia katika vyombo mbadala vya utatuzi vilivyotajwa na Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini Sura ya 318 *(Trustees Incorporation Act, CAP 318).* Mahakama Kuu ilitamka hivyo katika **KESI YA MADAI NAMBA 119 YA 2012 (CIVIL CASE NO 119 2012)** baina ya Wadai 19 na Kamati ya Muda ya Msikiti wa SUNNI MUSLIM JAMAAT DAR ES SALAAM. Wadai katika Shauri hili walikwenda Mahakama Kuu Dar es Salaam kujaribu kuzuia Kamati ya Muda ya Msikiti kufanya mkutano wa dharura ambao kimsingi hawa wadai walihofu kuwa huo mkutano ungegeuka kuwa wa uchaguzi wa viongozi.

Mahakama Kuu ilitamka kuwa Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini Sura ya 318 *(Trustees Incorporation Act, CAP 318)* imeweka mifumo imara ya utatuzi wa migogoro ndani ya taasisi za kidini mbadala wa kukimbilia Mahakamani kutatua migogoro kwa taratibu za kimahakama. Mahakama Kuu iliwaambia wadai kuwa hawakustahili kupeleka mgogoro wao bila kwanza kupitia

katika vyombo mbadala vya utatuzi vilivyotajwa na Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini.

Mahakama Kuu ilisema kuwa Kifungu cha 17 cha Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini kinatambua ngazi za usuluhishi wa migogoro mbadala au kabla ya kukimbilia Mahakamani. Ngazi hizo ni Mabaraza na Jumuiya za Kidini zilizosajiliwa chini ya sheria hii. Jumuia hizi ambazo zinatakiwa kupewa nafasi ya kusuluhisha ni pamoja na—BARAZA KUU LA WAISLAMU TANZANIA *(BAKWATA)*; BARAZA LA KIKRISTO TANZANIA *(CCT)*; BARAZA LA MAASKOFU TANZANIA *(TEC)*; *SEVENTH DAY ADVENTIST (SDA)*; BARAZA LA PENTEKOSTE TANZANIA *(PCT)* na wengine wengi.

**Mheshimiwa Rais**, Mgogoro ukishindwa kutatuliwa na Baraza la kidini husika, utapelekwa kwa Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu (Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini-RITA) atakayeongozwa na Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini kutatua huo mgogoro. Kazi za Mabaraza na Jumuiya za Kidini, na Kabidhi Wasii, ni kufanikisha usuluhishi na utatuzi wa migogoro mbali mbali, iwe kuhusu chaguzi, uongozi, miliki za ardhi na hata matumizi mabaya ya mali. Migogoro inapomfikia Kabidhi Wasii Mkuu, anaweza kutumia maafisa wake kufanya uchunguzi

na anaweza pia kumteua mtu mwingine yeyote afanye uchunguzi kwa niaba yake.

Katika KESI YA MADAI NAMBA 119 YA 2012, Mahakama Kuu Dar es Salaam ilisema kuwa huu utaratibu wa kuzitaka taasisi za kidini kutafuta usuluhishi kupitia vyombo vilivyotambuliwa na Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini inalenga kulinda uhuru wa kuabudu ndani ya taasisi za kidini na kuzikinga taasisi za kidini zisiingiliwe na Taasisi za Dola ikiwemo Mahakama. Kwamba, mamlaka ya Dola yanabaki katika kulinda uhuru wa kuabudu, kulinda amani na usalama wa watu wote.

### (c) Kituo Jumuishi Temeke: Nafasi ya Usuluhishi Katika Mashauri ya Ndoa na Mirathi

Baada ya mwaka mmoja wa kusikiliza mashauri ya ndoa na mirathi katika Mahakama Kuu – Kituo Jumuishi Temeke uzoefu umeonyesha kuwa usuluhishi unahitajika na unaweza kufanyika kwa ufanisi katika mashauri ya ndoa na mirathi. Kwa sasa, Sheria (Tangazo la Serikali Namba 196 la 1995) haliruhusu usuluhishi katika mashauri ya ndoa na mirathi.

*(i)-Usuluhishi Mashauri ya Ndoa*

Katika mashauri ya ndoa, Kifungu cha 101 cha Sheria ya Ndoa [Sura ya 29] kinataka mgogoro wa ndoa wenye madai ya talaka upitie kwenye Baraza la Kata la Usuluhishi kabla ya shauri kufunguliwa mahakamani. Hili likifanyika hakuna tena nafasi hiyo baada ya kesi kufika mahakamani. Hata hivyo katika kituo Jumuishi Temeke wadaawa wa mashauri ya ndoa wamekuwa wakieleza kuwa hawana ubishi kwamba ndoa yao imevunjika, hairekebishiki na wangependa mahakama itamke hivyo kwa makubaliano yao bila kupokea ushahidi. Maombi haya hukataliwa kwani kifungu cha 107 cha Sheria ya Ndoa kinataka ushahidi utolewe kuthibitisha ndoa yao imevunjika, hairekebishiki.

Uzoefu katika Kituo Jumuishi-Temeke unaonyesha kwamba, wadaawa wangependa kufikia muafaka kwenye masuala ya talaka. Hii imethibitishwa na tathmini iliyofanyika mwezi Novemba, 2022 ilionyesha kuwa katika rufaa za ndoa zinazofunguliwa Mahakama Kuu, warufani wengi hawalalamikii kuvunjwa kwa ndoa zao bali mgawanyo wa mali. Takwimu zilionyesha kuwa asilimia **73%** ya rufaa zinahusu malalamiko juu mgawanyo wa machumo ya ndoa, **10%** talaka na **17%** mambo mengine

kama Matunzo na Uangalizi wa mtoto. Uzoefu pia umeonyesha kwamba kuna kesi katika rufaa wadaawa hufika na mapendekezo ya jinsi ambavyo wangependa mali zao zigawanywe na huandika makubaliano *(settlement agreements)* ili iwe amri ya mahakama. Kwa mujibu wa Taarifa ya Kituo Jumuishi-Temeke, Mazingira haya yanadhihirisha umuhimu wa kurekebisha sheria iruhusu usuluhishi kwenye masuala ya ndoa ikijumuisha jinsi ambavyo wanandoa wangependa mgawanyo wa machumo ya ndoa uwe.

*(ii)-Usuluhishi Mashauri ya Mirathi*

Katika mashauri ya mirathi yapo maeneo mawili ambayo hubishaniwa sana na ambayo huchangia mashauri kuchelewa kukamilika Mahakamani. Suala la nani ateuliwe kuwa msimamizi wa mirathi. Hii hutokea pale ambapo warithi hawaelewani au baadhi yao hawakubaliani na wosia wa marehemu. Eneo lingine linalobishaniwa ni namna ya kugawana mali husika.

Kwenye eneo la nani ateuliwe msimamizi, hali hii husababishwa na dhana potofu iliyojengeka kuwa msimamizi wa mirathi ndiye mwenye mamlaka ya mwisho kuhusu ugawaji wa mali hata pale ambapo uamuzi wake

hautendi haki. Hata hivyo kuna mazingira (kesi za namna hiyo zipo tele) ambayo pande zinazosigana zikielimishwa, huondoa mapingamizi na kukubali upande mwingine uteuliwe kusimamia mirathi na hatua hii huharakisha kukamilika kwa shauri la mirathi.

Kwenye eneo la kugawa mali, shida imegawanyika katika sehemu mbili. Kwanza kutoridhika kwa binadamu na pili, upendeleo wa wazi unaoweza kufanywa na msimamizi wa mirathi. Katika hali zote mbili usuluhishi unawezekana kama utawekewa utaratibu unaodhibitiwa na mahakama, kama vile, mahakama kuwa na uamuzi wa mwisho pale ambapo kuna upande ambao hauridhiki na kinachofanywa na msimamizi wa mirathi au nani awe msimamizi wa mirathi baada ya usuluhishi kushindikana.

### *(iii)-Athari kwa Wajane na Watoto kwa Kukosekana Usuluhishi*

Athari kadhaa kwa wajane na watoto pale usuluhishi unakosekana. Athari hizi ni pamoja na watoto kulelewa kwenye mazingira ya migogoro na chuki. **Pili,** kucheleweshwa kwa haki ambapo malipo ya huduma kama ada za shule, matibabu na matunzo kwa Watoto havitapatikana kwa wakati. **Tatu,** kuharibika kwa mali

za marehemu kwa kukosa uangalizi. **Nne,** kutumia gharama kubwa kuendesha kesi. **Tano,** wajane kushindwa kutunza familia walizoachiwa na wenza wao. **Sita,** chuki zinazosabibishwa na kuwepo kwa mshindi katika kesi katika familia moja ambapo katika usuluhishi kila mmoja anajiona ni mshindi.

## 6. USULUHISHI NA UCHUMI

**Mheshimiwa Rais**, pamoja na jitihada za mahakama na wadau kuhakikisha mashauri yanayofikishwa mahakamani yanamalizika kwa wakati, ni dhahiri kuwa uendeshaji mashauri kwa njia ya kawaida hutumia muda mrefu na gharama ambazo zingeweza kuepukika endapo wahusika wangetumia njia mbadala za utatuzi wa migogoro yao. Pia, mashauri yanapoisha kwa njia ya usuluhishi, amani na undugu miongoni mwa wadaawa hudumishwa. Hii ni kutokana na kuwa wadaawa huamua mgogoro wao wenyewe badala ya jambo hilo kufanywa na hakimu au jaji. Uwepo wa amani ni chachu kubwa ya maendeleo ya kiuchumi ya mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Rais**, kuchelewa kukamilika kwa mashauri kuna athari za kijamii na kiuchumi. Kijamii, shauri linapochukua muda mrefu hadi kukamilika hupunguza nguvu ya uamuzi kubadili tabia katika jamii na hupunguza imani ya wananchi kwa mfumo wa sheria na kimahakama. Kuchelewa kukamilika hutoa nafasi kwa wadaawa wasio waaminifu kuwarubuni mashahidi.

Katika utendaji kazi wao, Majaji na Mahakimu wamekuwa wakipimwa na kutathminiwa kwa kuangalia

idadi ya mashauri yaliyosajiliwa, na yaliyomalizika. Kwa bahati mbaya baadhi ya Majaji, Mahakimu na Mawakili hawatafakari kwa kiasi gani shauri likichelewa lina athari za kijamii, kiuchumi na hata afya ya wadaawa.

Katika Kesi ya Madai Namba 218 ya Mwaka 1979 baina ya MAYALA GWEZO dhidi ya KARIM TRANSPORT, Mdai Mayala Gwezo alimuandikia Msajili wa Mahakama Kuu Dar es Salaam kulalamika kuhusu athari alizopata kutokana ucheleweshwaji wa shauri lake la madai.

Athari ya **kwanza,** alidai, alishindwa kuendelea na biashara yake kwa sababu mtaji wake ndio ulikuwa unabishaniwa Mahakamani kwa kuwa hakuweza kuutumia kuendeleza biashara yake. **Pili,** Kwa kushindwa kuendelea na biashara yake, familia yake ikavurugika kwa sababu ya matatizo makubwa ya kiuchumi yaliyomkabili yeye na familia yake na aliona dalili za ndoa yake kuvunjika. **Tatu,** matatizo haya yote yalimsababishia vidonda vya tumbo na mara kwa mara alikuwa akipata kiwewe na kuonekana kuchanganyikiwa kama vile mgonjwa wa akili.

# 7. WAJIBU WA WADAU KATIKA KUKUZA UTATUZI WA MIGOGORO KWA NJIA YA USULUHISHI KWA UCHUMI ENDELEVU

**Mheshimiwa Rais**, utafiti uliofanywa na Mahakama mwaka 2020 ulionesha changamoto kadhaa katika matumizi ya usuluhishi kama njia ya utatuzi wa migogoro. Changamoto hizo ni pamoja na baadhi ya mawakili kutochukulia kwa umakini zoezi la usuluhishi, dhana ya usuluhishi kutoeleweka vizuri miongoni mwa maafisa wa mahakama, wadaawa na mawakili; kutokuwepo kwa ujuzi wa kutosha miongoni mwa wasuluhishi, wadaawa kupendelea zaidi hukumu na tuzo za mahakama kuliko usuluhishi. Pia ni dhahiri kuwa wapo baadhi ya mawakili wenye mtazamo hasi dhidi ya usuluhishi kwa madai kuwa usuluhishi hupunguza kipato chao. Hawa wanaamini kuwa mgogoro unapochukua muda mrefu mahakamani huwapa faida zaidi kwakuwa wateja hulipa ada zaidi, gharama za kuhudhuria mahakamani, gharama za usafiri, posho za kujikimu na kuna baadhi ya mawakili huwatoza wateja wao kwa masaa wanayokaa mahakamani.

Mahakama tumejipanga kuongeza mafunzo kwa maafisa wa Mahakama na wananchi juu ya usuluhishi, kuendelea kuboresha Kanuni za usuluhishi na tumeufanyia mapitio

mwongozo wa mafunzo ya usuluhishi kwa maafisa wa Mahakama (*Mediation Training Manual for Judicial Officers*) ili kuendana na mabadiliko ya sheria.

Nichukue fursa hii kuwakumbusha mawakili wa kujitegemea kuwashauri wateja wao faida za usuluhishi na kutowalazimisha wateja wao kutumia njia ya kawaida ya usikilizaji wa mashauri hata pale ambapo wako tayari kusuluhishwa. Dhana kuwa wakitumia usuluhishi mapato yao yatapungua haibebi maslahi mapana ya nchi wala ya wateja wao.

**Mheshimiwa Rais,** nawapongeza, Chama cha Mawakili Tanganyika kwa kutambua umuhimu wa utatuzi wa migogoro nje ya mahakama na hivyo kuanzisha Kituo cha Kimataifa cha Uamuzi (**Tanzania International Arbitration Centre)** mnamo mwaka 2019. Kituo hiki kina mchango mkubwa katika kusaidia kujenga imani ya wawekezaji katika mfumo wetu wa utoaji haki kutokana na kusaidia kutatua migogoro ya kitaifa na kimataifa nje ya mahakama kwa haraka na kwa gharama nafuu.

## 8. MIFUMO YA KUONGEZA UFANISI KATIKA UTOAJI WA HUDUMA ZA MAHAKAMA

### (a)- MFUMO WA KUNUKUU NA KUTAFSIRI MIENENDO NA HUKUMU ZA MAHAKAMA (*transcription na translation software*)

**Mheshimiwa Rais**, Baada ya Uwekezaji Mkubwa uliofanywa na Serikali katika Miundombinu ya TEHAMA, Mahakama pia imeendelea kuunganishwa na Miundombinu ya TEHAMA na kuongeza matumizi ya TEHAMA katika utoaji haki. Tumeonyesha pia, wakati umefika wa Usuluhishi wa Migogoro kufanyika kwa Mtandao.

**Mheshimiwa Rais**, Kukamilisha safari ya Mahakama inayotoa huduma zake nyingi kwa njia ya Mtandao, tumekamilisha ujenzi wa MFUMO WA KUNUKUU NA KUTAFSIRI MIENENDO NA HUKUMU ZA MAHAKAMA (*transcription na translation software*). Mahakama ya Tanzania imekuwa ikitafuta software inayotumia *Artificial Intelligence* kutafsiri mienendo ya mashauri na hukumu za mahakama kutoka kiingereza Kwenda Kiswahili, na kutoka Kiswahili Kwenda Kiingereza. Tuligundua kuwa Mahakama ya Juu ya India

tayari ilikuwa inatumia software hii kutafsiri lugha kubwa tisa za India. Tulibaini kuwa, India walipata ujuzi huo kutoka Italia, nchi yenye utaalamu na uzoefu mkubwa wa kutengeneza program/softaware za kutafsiri na kuweka sauti katika maandishi *(translation and transcription).* Wataalamu wa Mahakama ya Tanzania, Mahkama Kuu Zanzibar, wakishirikiana na wale wa eGA; walikwenda Italia kutafuta na kufanikiwa kutengeza mfumo na kuufundisha lugha ya Kiswahili kwa lafudhi na sauti mbali mbali za Kitanzania.

**Mheshimiwa Rais**, Mfumo huu umejengwa kwa pamoja kati ya Mahakama ya Tanzania na mkandarasi *Almawave S.P.A* wa Italia kwa kutumia fedha za ndani. Utakapoanza kutumika, mfumo huu utawaondolea majaji na mahakimu jukumu zito la kunukuu na kutafsiri mienendo ya mashauri na hivyo kuongeza kasi ya usikilizwaji wa mashauri, uwazi na kuimarisha imani ya wananchi katika mahakama. Tanzania pia itapata mrahaba wa asilimia 20 kwa mauzo yoyote ya mfumo huu kwa mtu mwingine.

## (b)- MFUMO MPYA WA USIMAMIZI WA MASHAURI (ADANCED CASE MANAGEMENT SYSTEM)

**Mheshimiwa Rais**, Mahakama pia katika mwaka 2022 imekamilisha ujenzi wa mfumo mpya wa usimamizi wa mashauri (Adanced Case Management System) na tumendelea na mpango wa ununuzi wa compyuta mpakato *(laptop)* kwa ajili ya Mahakimu na Majaji wapya wote.

## (c)- MTAALA WA MAFUNZO YA AWALI YA WATUMISHI WOTE WA MAHAKAMA KUWAPA UWEZO WA KUTOA HUDUMA KIDIJITALI *(BASIC DIGITAL SKILLS CURRICULUM FOR JUDICIARY STAFF)*

**Mheshimiwa Rais**, Kusoma, Kuandika na kuhesabu (K-Tatu) hazitoshi katika karne ya 21 ambayo huduma za kimahakama zinahamia katika Mahakama-Mtandao (Mahakama ya Kidijitali). "K" ya nne, KUDIJITALI, ni muhimu kwa kila mtumishi wa Mahakama ya Tanzania. Ili safari ya kuelekea Mahakama-Mtandao au Mahakama ya Kidijitali ifanikiwe na iwe endelevu, watumishi wote wa Mahakama wanahitaji programu ya mafunzo ili wapate

kile kinachoitwa, *BASIC DIGITAL SKILLS* (ujuzi wa awali wa kufanya kazi na kutoa huduma katika mazingira ya kidijitali). Kikosi Kazi cha Mahakama kimekamilisha Rasimu ya Mtaala wa kuendeshea mafunzo endelevu kwa watumishi wote wa Mahakama *(BASIC DIGITAL SKILLS CURRICULUM FOR JUDICIARY STAFF)*. Baada ya kujadiliwa na kupitishwa, Mtaala huu utaanza kutumika.

## 9. SERIKALI ILIVYOIWEZESHA MAHAKAMA MWAKA 2022

**Mheshimiwa Rais**, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama nitashindwa kutambua uwezeshwaji mkubwa wa Mahakama uliofanywa na Serikali yako Mwaka 2022.

**Mheshimiwa Rais**, kwa mwaka 2022, uliendelea kuiongezea nguvu kazi Mahakama kwa kuteua Majaji 22 wa Mahakama Kuu. Uteuzi ulioufanya tarehe 6 Agosti 2022 uliongeza idadi ya Majaji wa Mahakama Kuu kutoka **78** hadi **100** na hivyo kupunguza mzigo wa mashauri kwa Mahakama Kuu kutoka mashauri **340** hadi **265** kwa wakati huo. Kutokana na ongezeko hili, kasi ya kumaliza mashauri kwa Mahakama Kuu imeongezeka kwa asilimia **1** kutoka asilimia **112** kwa mwaka 2021 hadi asilimia **113** kwa mwaka 2022. Hata hivyo kati ya Agosti 2022 hadi leo Majaji mawili wa Mahakama Kuu wamestaafu na mmoja kuaga dunia, hivyo kupunguza tena idadi ya majaji kutoka **100** hadi **97**.

**Mheshimiwa Rais**, kwa mwaka 2022, watumishi **292** wapya waliajiriwa wakiwemo Mahakimu Wakazi **48**. Ongezeko la idadi ya watumishi limesaidia pia Mahakama kutimiza mpango wake wa kusogeza huduma za mahakama karibu na wananchi kwa kuanzishwa kwa huduma ya

Mahakama Kuu katika Mkoa wa Manyara na huduma za mahakama katika wilaya 12 kufuatia kukamilika kwa mradi wa majengo ya Mahakama za Wilaya.

**Mheshimiwa Rais**, uwezeshaji mkubwa ulifanyika katika miundombinu ya majengo. Katika kipindi cha mwaka jana 2022 Mahakama ya Tanzania imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa majengo mapya **32** yakijumuisha majengo **24** ya Mahakama za Wilaya na 05 ya Mahakama za Mwanzo. Aidha majengo mengine 03 ya Mahakama yamefanyiwa ukarabati mkubwa.

**Mheshimiwa Rais**, ili kuendelea kusogeza huduma za Mahakama karibu na wananchi, kupitia mradi wa maboresho 2020/21- 2024/25 Mahakama inatarajia kufikisha huduma ya Mahakama Kuu katika mikoa nane isiyo na huduma hiyo ambayo ni **Singida**, **Pwani**, **Songwe**, **Katavi**, **Geita**, **Njombe**, **Simiyu** na **Lindi**. Aidha Mahakama inatarajia kujenga Mahakama za Mwanzo **60** na vituo jumuishi vya utoaji haki **10** kikiwemo kituo kimoja kitakachojengwa huko Pemba.

Kupitia fedha za ndani Mahakama imepanga kujenga jumla ya majengo **24** ambapo kati ya hayo, majengo **14** ni ya Mahakama za Wilaya na **10** ni ya Mahakama za mwanzo.

Kipekee nikushukuru sana wewe Mhe. Rais pamoja na serikali yote unayoiongoza mwishoni mwa Februari 2022, kwa kuridhia na kufanikisha Serikali kuingia katika makubaliano na Benki ya Dunia ya kuongeza fedha na muda wa utekelezaji wa mradi huu wa maboresho. Kukamilika kwa majengo hayo kutaongeza pia mahitaji ya watumishi. Ni matumaini yangu kwamba Serikali itaendelea kuiwezesha Mahakama kwa kutoa vibali vya ajira ili kusaidia wananchi kupata huduma za Mahakama karibu na maeneo yao, kwa gharama nafuu na kwa wakati.

**Mheshimiwa Rais**, mwaka 2022 Mahakama imeendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama-Dodoma. Hadi sasa ujenzi huu umekamilika kwa asilimia 80 na unategemewa kukamilika kabisa ifikapo 30 Machi, 2023. Katika kutimiza lengo la Mahakama kuhamia Dodoma baadhi ya watumishi wa Makao Makuu ya Mahakama wameshahamia Jijini Dodoma na wanaendela na shughuli zao za kila siku katika jengo letu jipya la Makao Makuu huku ujenzi ukiendelea katika maeneo machache yaliyobaki. Awamu ya kwanza ya watumishi 31 wako Dodoma tangu 27 Desemba, 2022. Kufikia mwishoni mwa mwaka huu wa fedha yaani Juni, 2023, watumishi wote manaopaswa kuhamia makao makuu ya mhimili wa Mahakama watakuwa wamehamia Dodoma. Niendelee

kuishukuru sana Serikali kupitia Hazina kwa kuhakikisha kwamba fedha za ujenzi zinatolewa kila zinapoombwa.

**Mheshimiwa Rais**, Mahakama pia inaendelea na mradi wa ujenzi wa nyumba za majaji wa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu hapa Dodoma wenye thamani ya shilingi **42,785,988,380.87** na ujenzi unategemea kukamilika ifikapo tarehe 19 Mei, 2023. Haikuwa kazi nyepesi kutekeleza miradi hii mikubwa ya ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama pamoja nyumba za majaji kwa wakati mmoja na kwa kupitia fedha za ndani. Nichukue tena fursa hii kuipongeza Serikali yako kwa kuhakikisha fedha kwa ajili ya miradi hii mikubwa zinapatikana.

## MWISHO:

**Mheshimiwa Rais,** napenda kumalizia kwa kukushukuru kipekee wewe kwa kukubali kuwa mgeni rasmi katika SIKU YA SHERIA NCHINI kwa mwaka huu wa 2023. Kwa heshima na taadhima naomba sasa nikukaribishe utupatie nasaha zako za SIKU YA SHERIA NCHINI kwa mwaka 2023.

## KARIBU SANA MHE. RAIS

THE JUDICIARY OF TANZANIA

MAHAKAMA YA TANZANIA